Masalio na Utume Wake

“Kanisa la ulimwenguni linajumuisha wale wote ambao kwa kweli wanaoamini katika Kristo lakini katika siku za mwisho wakati wa kuenea kwa uasi, watu wa masalio wameitwa watoke wazitunze amri za Mungu na imani ya Yesu. Hawa masalio wanatangaza saa ya kuja kwa hukumu, wakihubiri wokovu katika Kristo, na kupiga mbiu ya kukaribia kuja kwake mara ya pili. Tangazo hilo linawakilishwa na mfano wa malaika watatu wa Ufunuo 14; linaambatana na kazi ya toba na matengenezo duniani. Kila muumini anatakiwa binafsi kuwa na sehemu katika ushuhuda huu wa ulimwenguni mwote.” (Uf. 12:17; 14:6-12; 18:1-4; 2Kor.5:10; Yuda 3, 14; 1Pet. 1:16-19; 2Pet.3:10-14; Uf. 21:1-14)

Joka limeangusha theluthi ya malaika na linavizia mtoto azaliwe na mwanamke ili amle.Likiweza, litakuwa limeshinda vita. (Uf.12:4, 7-9). Joka linarukia lakini mtoto ananyakuliwa na Mungu. Mwanamke anajificha nyikani kwa muda wa miaka $3\frac{1}{2}$ (Uf. 12:6, 13, 14). Kwenye Biblia, Mwanamke ni Kanisa (2Kor. 11:2) na Joka ni Shetani (Uf.12:9). Pale msalabani, Kristo alimshinda Shetani (Yoh. 12:31). Mbingu ziliimba wimbo, Shangilieni enyi mbingu (Uf. 12:10, 11) na kwa dunia kukatangazwa ole (Uf. 12:12). Ili kutuliza hasira zake, Joka amekuwa akimsumbua mwanamke (Uf. 12:13) na mwanamke alijificha nyikani. Baada ya miaka 1260, Joka anakasirikia masalio, na kufanya vita na wazao wake waliosalia (Uf. 12:17). Sasa lini mambo hayo yalitokea, lini masalia walianza kuonekana, ni nini utume wa masalio? Haya ndiyo tunayotakiwa kujifunza.

Uasi Mkuu

Mateso kwa watu wa Mungu, kwanza yaliletwa na utawala wa Rumi ya kipagani. Yesu alionya angalieni mtu asiwadanganye na watazuka makristo wa uwongo ambao wangedanganya hata wateule. (Mt. 24:4, 24). Wafuasi wake wangekabiliwa na mateso makali (Mt. 24:21, 22). Zitakuwako ishara juu ya nchi zitazodhihirisha kukoma kwa mateso na kukaribia kuja kwa Yesu (Mt. 24:29, 32, 33). Paulo naye alionya akishaondoka, watazuka mbwa mwitu wasilihurumie kundi (Mdo. 20:29, 30). Uasi lazima utokee kabla Yesu hajarejea (2Thes. 2: 3, 4) na hata siku za Paulo, siri ilikuwa inatenda kazi (2Thes. 2: 7, 9, 10). Yohana alisema itazuka roho ya mpinga Kristo nayo tayari ilikuwapo (1Yoh. 4:1, 3).

Kuinuka kwa Mtu wa Kuasi

Kanisa lilipoacha upendo wake wa kwanza (Uf. 2:4), liliacha usafi wa mafundisho, viwango vya juu vya maisha ya kikristo na kufutilia mbali mivuto ya Roho Mtakatifu. Umaarufu na uwezo binafsi wa watu vikaanza kutumika kuchagua viongozi. Usimamizi wa Kanisa chini ya Roho Mtakatifu uliachia urasimu wa kikasisi chini ya Askofu ambaye ulimweka chini yake kila mshiriki wa kanisa. Hivyo uongozi wa Kanisa ukafikiriwa ni utawala wa Kanisa na mkuu akakoma kuwa mtumishi wa wote badala yake akafanywa mpatanishi wa mwanadamu na Bwana. (SDA Bible Commentary 4 uk. 385). Chini ya mfumo wa Upapa, kanisa la kikristo lilizama kwenye uasi zaidi. Mwaka 533, Kwenye Amri za Justianian, iliwekwa ibara ya kumtambua Askofu wa Rumi kama kiongozi wa makanisa yote ulimwenguni pamoja na uwezo wake wa kuwatenga wazushi. Mwaka 538, Askofu wa Rumi alipata uhuru zaidi baada ya utawala wa Ostrogoth kuondoshwa. Hivyo akapata madaraka zaidi kutumia waraka wa Justinian wa mwaka 533. Hivyo mwaka 538BK ilianza miaka 1260 ya mateso ya watu wa Mungu iliyotabiriwa (Dan. 7:25, Uf. 12:6, 14; 13: 5- 7). Wengi waliacha imani yao kwa hofu.

Kabla ya matengenezo, sauti zilisikika ndani ya kanisa zikipinga kuua waprotestanti pasipo huruma, madai ya uwongo ya mamlaka ya kanisa na ufisadi. Hatimaye mwaka 1798, Kanisa Katoliki lilipata jeraha la mauti (Uf. 13: 3). Berthier, Jemedari wa Napoleon, alifika Rumi na kumteka Papa Pius wa sita, ambaye alifia uhamishoni. Makanisa mengi ya kiprotestanti yalitafsiri jambo hili kama utimilifu wa unabii.

Matengenezo

Mafundisho yasiyofuata Biblia ndiyo yaliyoshusha hali ya kiroho ya kanisa. Baadhi ya mafundisho ya uwongo ni kama haya yanayotajwa hapa: -

1. Kiongozi wa Kanisa duniani kuhesabika kuwa mwakilishi wa Mwana wa Mungu duniani. Hili hudai kwamba Askofu wa Rumi pekee ndiye mwakilishi wa Mwana wa Mungu duniani (cf. Mt. 23:9)
2. Kanisa halikosei wala kiongozi wake hawezi kukosea – Kanisa linadai halijapata kukosea wala halitakaa likosee (c/f. Uf. 14: 8, Uf. 18:1-3)
3. Wokovu kupatikana kupitia kwa kanisa peke yake. Hoja hii hujaribu kuzima huduma ya Yesu ya Upatanisho (c/f Ebr. 4:16)
4. Matendo mema husaidia kufuta dhambi zilizofanywa baada ya ubatizo (c/f Rum. 3: 20)
5. Mamlaka yote iko kwenye Kanisa Katoliki na kwamba mapokeo na maandiko yana mamlaka sawa (c/f 2Tim. 3:16 na sola scriptura)

Kuanzia karne ya 14 wanamatengenezo waliinuka wakiwamo John Wycliffe, Martin Luther, kwa nguvu wakilitambulisha Kanisa Katoliki kuwa ni pembe ndogo ya Daniel 7: 25 na mnyama wa Ufunuo 13: 1-10, aliyetesa watu wa Mungu kwa miaka 1260 (Uf. 12: 6) Wanamatengenezo walipinga ibada za watakatifu kama Maria, pagatori, namna ya kuadhimisha Meza ya Bwana na mafundisho ya uwongo yaliyoorodheshwa hapo juu.

Kushindwa kuendelea na matengenezo

Matengenezo yasingekoma kwenye karne ya 16. Yalikuwa yamefanya kazi kubwa ila hayakukamilisha kuileta nuru ya Biblia yote kanisani. Mafundisho ya ubatizo wa kuzamisha majini, kutokufa kama zawadi itakayotolewa na Yesu arudipo mara ya pili, Sabato ya siku ya saba kama ndiyo sabato ya Biblia, kuadhimisha meza ya Bwana kwa kutawadhana miguu, yaliachwa gizani. Mashindano yakazuka, na hapakuwa na kipindi ambacho makanisa yalikuwa yakionyeshana makosa kama hiki.

Masalio

Pamoja na uasi na mateso ya miaka 1260, baadhi ya washiriki waliendelea kuakisi usafi wa kanisa la mitume. Wakati mateso yalipokoma 1798, Joka alikuwa ameshindwa kufutilia mbali watu wa Mungu waaminifu. Yohana anasema, Joka akamkasirikia mwanamke, akaenda zake kufanya vita na wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu (Uf. 12:17).

Masalio ni akina nani? Yohana anawaita uzao uliosalia (Uf. 12:17), ikiwa na maana ya mabaki. Biblia inawaonyesha kuwa ni kundi la watu wa Mungu ambao pamoja na majanga, vita na uasi, bado wamebaki kuwa watiifu kwa Mungu kiukamilifu. Hawa ndio wanaotumika kupandikiza kanisa la Mungu linaloonekana ulimwenguni (2Nyak. 30:6; Ezr. 9:14, 15; Isa. 10: 20-22; Yer. 42:2; Eze. 6:8; 14:22).

Mungu aliagiza masalio watangaze haki yake ulimwenguni na mlima Sayuni (Isa. 37:31, 32; 66: 20 c/f Uf. 14:1) Hawa ndio wamfuatao Mwana Kondoo kila aendako (Uf. 14:4).

Tabia za masalio:

1. Wana imani ya Yesu (Uf. 14:12). Wanatangaza habari njema kama ushuhuda kwa wanadamu (Uf.14: 6, 7; 10:11 Mt. 24:14)
2. Wanatii amri za Mungu – Wanaenenda kama Yesu (1Yoh.2:6), Wanatii amri za Mungu kama Yesu (Yoh. 15:10). Kwa kuwa ni masalio, matendo yao lazima yafanane na imani yao la sivyo si kila mtu amwitaye Yesu atauona uzima (Mt. 7:21). Kwa neema waliyopewa na Kristo, wanatii amri za Mungu zisizobadilika (Kut. 2o: 1- 17; Mt. 5: 17-18; 19: 17; Wafil. 4:13)
3. Wana ushuhuda wa Yesu ambayo ni Roho ya Unabii (Uf. 19:10). Ni kazi ya Roho kwa njia ya karama kuukamilisha mwili wa Kristo hadi utimilike (Efe. 4:12, 13).
4. Kuinuka kwake, kunakuja baada ya miaka 1260 yaani baada ya mwaka 1798 na kushambuliwa na Shetani (Uf. 12:6, 17).

Utume wa Masalio

Unabii wa Ufunuo hudhihirisha utume wa Masalio. Kutangaza ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14: 6 - 12 kurejesha ukweli wa injili kabla Yesu hajarejea. Hili ni jibu la Mungu kwa uwongo wa Mnyama wa Ufu. 13:3, 8, 14-16). Baada ya onyo kutolewa, Yesu atarejea (Uf. 14:14-20).

Ujumbe waMalaika wa Kwanza (Uf. 14:6, 7). Injili ya milele ni habari ile njema iliyohubiriwa na mitume (Ebr. 4:2). Ujumbe unauita ulimwengu utubu (Mith. 8:13)na kuzaa matunda (Yoh. 15:8). Pia tumeitwa kumtukuza Mungu katika miili yetu (1Kor. 6:19, 20) au kwa chakula, vinvywaji na yoyote tutakayotenda (1Kor. 10:31). Hukumu inamaanisha mchakato wote wa uchunguzi hadi kufikia kuachiliwa au kupewa kifo (mt.16:27, Rum. 6:23 na Uf. 22:12). Saa ya hukumu pia yatangaza hukumu ya Mungu kwa uasi (Dan. 7:9-11, 26 na Uf. 17, 18). Ujumbe wa malaika wa kwanza pia unatuita kumwabudu Muumbaji aliyeumba mbingu na nchi na chemichemi za maji (Uf.14:7 c/f Kut. 20:11). Hivyo ujumbe huu unauita ulimwengu kuikumbuka sabato ya siku ya saba ya juma. Hatimaye, ujumbe huu hurejeza sheria ya Mungu iliyovunjwa na mtu wa kuasi (2Thes. 2:3).

Kwa ufupi, Mungu anaita wanadamu wamwabudu katika roho na kweli. Ndiye aliyewaumba na ndiye aliyewakomboa

Ujumbe wa Malaika wa Pili (Uf.14:8) Tangu awali, jiji la Babeli lilijidhihirisha kuwa kinyume na Mungu. Mnara wake ulikuwa kituo cha uasi (Mwa. 11:1-9), Lusifa (Shetani) alikuwa kiongozi wake asiyeonekana (Isa. 14;4, 12 -14)na alitaka kuifanya Babeli kuwa kiongozi wa kutawala d

Ujumbe wa Malaika wa Tatu (Uf. 14:9-12) Ujumbe wa malaika wa tatu ni onyo kali la Mungu kwa wanadamu ambao watakuwa wanahimizwa kuabudu ibada ya uwongo. (Uf. 13:1-18). Mnyama wa kwanza (Uf. 13:1-10) anaelezea muungano wa serikali na kanisa uliotawala dunia kwa karne nyingi ((1Thes. 2:2-4; Dan. 7:8, 20-25; 8:9-12). Sanamu ya mnyama inawakilisha dini ya uasi wakati makanisa ya matengenezo yatakapoungana na serikali tena na kuanza kutesa watakatifu kama ilivyotokea kwa miaka 1260. Ujumbe wa malaika wa tatu ni onyo kali. Hatimaye, suala la ibada ya kweli na ya uongo ndiyo yatakuwa masuala yanayohusu pambano kuu. Uchaguzi siyo rahisi, kwa kuwa atakayechagua Joka, atakutana na ghadhabu ya Mungu na atakayemchagua Mungu atakutana na hasira za Joka (Uf.12:17). Hata hivyo, hatimaye Joka atapokea mapigo saba na kutupwa kwenye ziwa la moto (Uf. 15, 16; 20:14, 15). Mungu anataka tumwabudu katika roho na katika kweli (Yoh.4:23) na hapokei ibada ya uongo (Mt.15:8, 9). Kwa sasa anawaita walio Babeli watoke wamfuate (Uf.18:4)

Kwa ufupi, ghadhabu ya Mungu inaelekezwa kwa wanadamu wanaokataa mpango wake (Yoh. 3:17, 18, 36)

==========Mwisho wa Somo========

Swali: Je Jumamosi huwakilisha muhuri wa Mungu na Jumapili alama ya mnyama? Hii ni kwa sababu katika Kitabu cha Tumaini Kuu Sura ya 25 kuna maneno yafuatayo: “Kanisa la Rumi linakiri kuwa wao ndio walibadili sabato, na kusema kuwa Waporotestanti wanapokubali kushika siku ya Jumapili kama siku ya ibada, wanayatambua mamlaka yao. Wao husema: “Sheria ya zamani, yaani sabato, ndiyo iliyotakaswa; lakini kanisa letu likiagizwa na Yesu na Roho wa Mungu, limebadili sabato ya Jumamosi na kuweka Jumapili badala yake. Sasa tunatakasa siku ya kwanza, wala sio siku ya saba. Hivyo sasa Jumapili ndiyo siku ya Bwana” Ili kuonyesha uwezo au mamlaka yao, wafuasi wa Rumi huandika kwamba kule kubadili sabato na kwenda jumapili badala yake, ambavyo hata Waprotestanti wanakubali kushika, huonyesha uwezo wa kanisa kuamuru sikukuu na kuamuru ushikaji wake chini ya dhambi. Basi kubadili sabato kuna maana gani basi, isipokuwa kuonyesha uwezo au alama ya mamlaka ya kanisa la Rumi?”

Jibu. Hili ni swali ambalo linahitaji somo lake linalojitegemea. Hapa jitihada inafanywa kujibu kidogo.

Muhuri huwakilisha mamlaka (Esta 8:2). Paulo anasema “Lakini msingi wa Mungu ulio mathubuti umesimama ukiwa na muhuri wenye maandishi haya: ‘‘Bwana anawajua walio wake’’ tena, ‘‘Kila alitajaye jina la Bwana auche uovu.’’ (2Tim.2:19). Hivyo Mungu kuwajua walio wake na wafuasi kuacha uovu ni mambo mawili makubwa kabisa. Sabato iliwekwa kuwa ishara ya uumbaji wa Mungu (Mw. 2:1-3; Kut. 20:11 Kut. 31:17; Eze. 20:20). Sabato pia ni ishara ya kuokolewa (Kut. 31:13, Eze. 20:12). Inawezekana kabisa Mungu anawajua walio wake kwa kuwa aliwaumba, na pia kwa kuwa ni watoto wake, wanaitwa kuacha uovu. Hivyo tunaogundua kwamba kile ambacho Sabato ya siku ya saba husimamia, kinajiakisi katika maelezo ya muhuri.

Muhuri hupatikana kwenye sheria. Zaidi ya yote, huonyesha mtoa sheria, madaraka yake na mipaka ya utawala unaohusika. Biblia nayo huonyesha kwamba muhuri unahusiana na sheria ya Mungu "Funga ushuhuda na kutia muhuri sheria miongoni mwa wanafunzi wangu" (Isa. 8:16). Zaidi ya yote imesisitizwa "Na waende kwa sheria na ushuhuda, kama hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa ho hapana asubuhi (Isa.8:20). Kwamba Sabato imewekwa katikati ya Sheria ya Mungu, inaipa uzito hoja kwamba sabato ndiyo muhuri.

Sabato na Jumapili, huwakilisha mifumo miwili tofauti, ukweli na uwongo, haki kwa imani na haki kwa matendo, njia ya Mungu na njia ya mwanadamu. Ijulikane kwamba mifumo hii miwili kwa sasa haitofautishi wanadamu wanaokaa duniani. Njia ya Mungu ya wokovu ni ya kupata haki kwa imani (Efe. 2:8-10). Njia ya mwanadamu ya kupata wokovu ni ya kufuata matendo ya sheria (Gal. 3:11).

Wako wakristo wengi wanaoabudu siku ya Jumapili waliokwisha onja pumziko kwa kadiri ya nuru waliyonayo; (Rum. 2:14-16) na wapo miongoni mwa waabuduo siku ya sabato ya siku ya saba ya juma ambao hutegemea matendo yao kwa wokovu (Ebr.4:4-6).

Zaidi ya yote "Ni vigumu sana kuuchora mstari wa kutenganisha walio wakristo wasio wa Mungu. Washiriki wa Kanisa hupenda ulimwengu upendacho na wako tayari kushirikiana nao." (GC588).Wakati Ujumbe wa Malaika Watatu utakapohubiriwa kwa uwazi na kuunganisha na siku za ibada,(Uf.18:1-4) ndipo siku za Sabato na Jumapili zitakapowakilisha mifumo miwili.

Kwa ajili ya kujibu swali lililoulizwa, bado Jumapili haijawa alama ya mnyama kwa kuwa utaratibu wa namna ya kuokolewa havijaunganishwa na siku mbili tunazozungumzia. Bado kuna utata. Hivyo, kwa sasa, haileti maana kuhitimisha kwamba wanaosali Jumapili wamekwisha pokea alama ya mnyama.

Hoja itakayoshindaniwa ni ukweli. Kabla ya mwisho wa wakati, ujumbe wa haki kwa imani utahubiriwa kwa nguvu (Mt. 24:14). Sabato itawakilisha haki kwa imani kutokana na kile Yesu alichotutendea na Jumapili itawakilisha wanaotegemea matendo yao kuokolewa. Kwa upande mwingine, bado ibada haijaanza kulazimishwa kwa kufuata utaratibu wa serikali. (Uf.13:11-18). Wakati dunia itakapolazimisha utaratibu wake wa ibada, na wanadamu wakaacha kumtii Mungu, wakafuata inachoagiza dunia, ndipo watakapopokea chapa ya Mnyama. Watakaokataa mpango wa Mungu, wakapokea chapa, hao ndio watakaokabiliwa na ghadhabu yake (Yoh. 3:36; Ufu. 14:9-11).

"Wakristo wa zamani walishika jumapili wakidhani kuwa walikuwa wakishika sabato ya Biblia, … 'Jumapili iliwekwa na Mungu'. Watu hao Mungu hupokea ibada zao na uaminifu wao. Lakini wakati amri ya Jumapili itakapowekwa kisheria, ulimwengu utaangazwa na kuiona sabato ya kweli, ndipo hapo wale watakaoasi amri ya Mungu na kuendelea kushika Jumapili iliyowekwa na Rumi, watakuwa wanaheshimu Rumi badala ya Mungu. Watakuwa wanamwabudu mnyama na sanamu yake. Basi watakuwa wanaipokea ishara ya Rumi – yaani alama ya mnyama. Bado mpaka amri ya jumapili itakapowekwa, ndipo watu watachagua kati ya kumtii Mungu au mwanadamu, na wale watakaoendelea kumwasi Mungu watapokea "alama ya mnyama". Pambano Kuu Ktb II uk. 94.